

**Na: 14. Msimu wa Kilimo 2017/18 Tathmini ya kipindi cha Februari 11-20, 2018 na matazamio kwa kipindi cha Februari 21-28, 2018**

**MUHTASARI**


- Wakulima katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wanaendelea na shughuli za palizi.
- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua wanaendelea na shughuli za uvunaji wa mazao isipokuwa katika mkoa wa Shinyanga ambapo mahindi yapo katika hatua ya kukomaa.
- Wakulima wanashauriwa kuzitumia siku ambazo hazina mvua kwa shughuli za palizi

**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA  
KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2018**

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika kidogo wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kushuka kusini zaidi mwa Tanzania. Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la chini ya wastani hadi wastani. Kwa upande mwingine kumekuwepo na joto la bahari la juu kidogo ya wastani katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI  
CHA FEBRUARI 11-20, 2018**

Katika kipindi cha siku kumi maeneo mengi ya nchi yalipata mvua za chini ya 50% ya wastani wa muda mrefu kwa kipindi cha siku kumi kama inavyoonekana kwenye kielelezo. Hata hivyo, mvua zaidi ya 80% ya wastani wa muda mrefu kwa kipindi cha siku kumi zilinyesha katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mara, Pwani, Shinyanga, Simiyu, Kigoma, Iringa kusini na mashariki mwa mkoa wa Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.



Kielelezo. Kiasi cha mvua (%) kipindi cha Tarehe 11-20 Februari, 2018

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA  
KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2018**

Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima wanaendelea na palizi wakati maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua uvunaji wa mazao unaendelea isipokuwa katika mkoa wa Shinyanga ambapo mazao yapo katika hatua ya kukomaa. Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua wakulima wameanza kuandaa mashamba hususan mkoa wa Kagera. Hali ya maji na malisho ilikuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi isipokuwa baadhi ya maeneo ya mkoa wa Arusha hususan katika wilaya ya Longido.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2018

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka hususan katika mabonde ya Rufiji, Ruvuma, Nyasa na Rukwa kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2018

**M**igandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kubaki katika maeneo ya kusini mwa Tanzania. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi na hii inatarajiwa kusababisha upepo kuvuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi. Kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la juu kidogo ya wastani hadi chini ya wastani.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2018

**K**anda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua za wastani katika maeneo machache hususan kati ya tarehe 24 hadi 28 Februari, 2018.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Maneno hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2018

**M**vua zinazotarajiwa zitasaidia kuongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya ukuaji wa mazao na malisho. Wakulima wanashauriwa kuzitumia siku ambazo hazina mvua kwa shughuli za palizi. Maji na malisho kwa mifugo vinatarajiwa kuimarika kwenye maeneo mengi ya nchi. Wakulima, wavuvi, na wafugaji wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani husika kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2018

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka kidogo katika mabonde ya Rufiji, Ruvuma, ziwa Tanganyika na bonde la kati kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz) (2) [agromet@meteo.go.tz](mailto:agromet@meteo.go.tz);

Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)